## Maswali

1. Malaika aliambia Mariamu nini?
2. Malaika aliambia Yusufu nini?
3. Mbona Mariamu na Yusufu walienda Bethlehemu?
4. Hakukuwa na nafasi kwa chumba cha wageni. Mariamu alienda kupumzika wapi?
5. Marimu aliweka wapi mtoto Yesu?
6. Nani waliona malaika wengi angani?
7. Mamajusi walifuata nini?
8. Mamajusi walienda kwanza wapi kuona mtoto mfalme?
9. Agano la kale ilisema kwamba Kristo atazaliwa wapi?
10. Mtoto Yesu alihepa Herodi mfalme mbaya namna gani?

## Majibu

1. Malaika aliambia Mariamu kwamba atakuwa na mtoto asiye wa kawaida –Mwana wa Mungu.
2. Malaika aliambia Yusufu amuoe Mariamu. Mtoto wake ni Mwana wa Mungu.
3. Kaisari alitengeneza sheria kwamba kila mtu aende kwa mji wa jamii yao kujiandikisha.
4. Mariamu alienda kupumzika kwa boma.
5. Marimu aliweka mtoto Yesu kwa hori.
6. Wachungaji waliona nyota nyingi angani.
7. Mamajusi walifuata nyota isiyo ya kawaida.
8. Mamajusi walienda kwanza Yerusalemu mji mkuu.
9. Agano la Kale ilisema Kristo atazaliwa Bethlehemu.
10. Malaika aliambia Yusufu atoroke aende Misri pamoja na Mariamu na mtoto Yesu.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 2 Mwaka wa 1

# 33 Kuzaliwa kwa Yesu

**Kwa Biblia** Matayo 1:18-25 na 2:1-18

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Yesu ni mwana wa Mungu tena ni mwana wa Mariamu. Yeye ndiye mfalme aliyechaguliwa na Mungu, lazima tumtumikie.

### Somo

Mariamu aliishi kwa kijiji cha Nazareti. Alikuwa ameposwa kuoleka kwa Yusufu seremala. Siku moja Mariamu alikuwa na shuguli za kufanya kazi za nyumbani. Mara tu akaona mtu amesimama karibu naye. Mariamu alishtuka na kuogopa. Yule mtu alimwambia, “Mariamu, usiogope, nimekuletea habari kutoka kwa Mungu.” Halafu Mariamu akafahamu kwamba anazungumza na malaika.

Malaika alimwambia kwamba atakuwa na mtoto asiye wa kawaida. Atakuwa mtoto wa Mungu. Mwana huyu wa Mariamu atakuwa mkuu na atakuwa mfalme kwa kiti cha enzi cha mfalme Daudi kule Yerusalemu. Atatawala Israeli milele.

Malaika alipoondoka Mariamu aliwaza sana juu ya maneno aliyoambiwa. Mariamu alikumbuka ahadi zenye Mungu alisema kwa Agano la Kale.Mungu alikuwa ameahidi kwamba mtoto asiye wa kawaida atazaliwa na kuleta baraka kwa watu wote duniani. Mungu alikuwa ameahidi kwamba atatawala ulimwengu mzima milele. Mungu aliahidi kwamba huyu mtoto atakuwa mwanawe halisi. Ni habari ya ajabu aje aliyoleta malaika kwa Mariamu! Mungu alimchagua Mariamu kuwa mama halisi wa mwanawe.

Mariamu alienda kuishi na binamu wake Elisabeti. Aliambia Elisabeti kwamba alikuwa anatarajia mtoto asiye wa kawaida. Mtoto wake atakuwa mwana wa Mungu. Mariamu alikaa na Elisabeti kwa miezi mitatu. Halafu akarudi nyumbani Nazareti.

Yusufu alipoona Mariamu na mimba, aliogopa. Yusufu hakufurahia, alifikiri Mariamu amemdakanya. Lakini usiku moja malaika alimkujia Yusufu kwa ndoto. Mtoto mwenye Mariamu anatarajia ni mwana wa Mungu. Malaika alimwambia Yusufu amuoe Mariamu. Mungu alikuwa amemchagua yeye kulinda Mariamu na mtoto huyo. Kwa hivyo Yusufu na Mariamu walioana.

Kaisari aliweka sheria kwamba kila mtu lazima aende kwa mji wake ajiandikishe kwa ajili ya kodi. Bethlehemu ulikuwa mji wa Yusufu na Mariamu. Yusufu na Mariamu walisafiri mwendo mrefu kuenda Bethlehemu. Mtoto wa Mariamu alikuwa karibu kuzaliwa.

Mwishowe walifika Bethlehemu. Yusufu alihofia Mariamu. Alikuwa amechoka sana. Bethlehemu kulijaa watu. Watu wengi walikuwa wamekuja kujiandikisha. Yusufu aliendа ndani ya chumba cha wageni kutafutia Mariamu mahali apumzike. Lakini ndani kulijaa watu. Hakukuwa na chumba cha wao kulala.

Yusufu alijua kwamba mtoto wa Mariamu karibu atazaliwa. Mlinzi wa chumba cha wageni alikuwa mzuri. Hakukuwa na kitanda chao cha kulalia. Lakini aliambia Yusufu wapumzikie kwa boma. Yusufu alishukuru huyo mlinzi. Aliongoza Mariamu kupita ndani ya wale watu wengi. Alimtengenezea mahali miongoni mwa wanyama.

Baadaye mtoto wa Mariamu alizaliwa. Mwana wa Mungu alizaliwa kwa boma ya n'gombe miongoni mwa wanyama. Mariamu alifunga mtoto kwa nguo zake na kumweka ndani ya hori. Mtoto aliitwa Yesu. Kulikuwa na wachungaji wakichunga kondoo kando ya vilima nje ya mji wa Bethlehemu. Baadaye usiku huo, malaika alionekania wale wachungaji. Utukufu wa Mungu uliwaka angani. Malaika aliambia wachungaji, " Namletea habari njema ya furaha. Mwokozi amezaliwa Bethlehemu. Ni Kristo, ni Bwana. Mtapata huyu mtoto amefungwa ndani ya nguo za mtoto na amelazwa horini." Papo hapo malaika wakatokezea angani wakisifu Mungu.

Malaika walipoondoka, wachungaji walienda ndani ya Bethlehemu. Walipata Marimu na mtoto aliyekuwa amelala horini. Wachungaji walishukuru Mungu kwa kuona mtoto asiye wa kawaida. Walirudi kwa kondoo wao wakisifu Mungu kwa sababu ya yote waliyoona na kusikia.

Kulikuwa na mamajusi walioishi mbali upande wa mashariki. Hawa mamajusi waliona angani nyota isiyo ya kawaida. Walifuata hiyo nyota ili wampate mtoto aliyezaliwa kama mfalme wa Wayahudi. Mamajusi walienda mpaka Yerusalemu, mji kuu. Mfalme Herode alitawala Yerusalemu. Alikuwa katili tena wa wivu.

Mamajusi walikuja kwa Mfalme Herodi. Wakamuuliza, "Wapi aliyezaliwa kama mfalme wa Wayahudi?" Mfalme Herodi alituma wawaite makuhani na walimu. Aliwauliza wapi patazaliwa Kristo. Manabii wa Agano la Kale waliandika juu ya ahadi za Mungu kuhusu kuja kwa mfalme. Makuhani waliambia Mfalme Herodi, "Kristo atazaliwa Bethlehemu." Herodi alituma mamajusi waende waone mtoto. Alijifanya kwamba yeye naye anataka kwenda kumsujudia mtoto. Aliambia mamajusi warudi wamwambie penye anaweza kupata mtoto.

Mamajusi walipokuwa wakienda, hiyo nyota ilionekana tena. Nyota iliwaongaza mpaka penye Mariamu na mtoto walikuwa. Mamajusi waliinama na kumsujudia Yesu. Walimpa zawadi ya dhahabu, uvumba na manemane.

Mungu alihadharisha mamajusi kwa ndoto kwamba wasirudi kwa Herodi. Walirudi nyumbani kupitia njia nyingine. Halafu malaika akaonekania Yusufu usiku kwa ndoto. Akasema, "Amka, chukuwa mtoto pamoja na mamake mtorokee Misri. Makae huko mpaka nitakapo mwambia kwa sababu Herodi atatafuta mtoto akitaka kumuua." Yusufu aliamka upesi wakasafiri kuenda Misri na Mariamu pamoja na Yesu.

Mfalme Herodi alikasirika sana aliposikia kwamba kulikuwa na mfalme mwingine. Alikasirika tena kwa sababu mamajusi hawakurudi kwake. Herodi alituma askari Bethlehemu waue watoto wavulana wote. Lakini Yesu alikuwa nchi ya Misri salama. Yusufu alikaa huko mpaka Herodi akafa.